Kwa maoni wasiliana na Tume
kupitia anuani ifuatayo:

Katibu Mtendaji,
Tume ya Kurekebisha Sheria
Tanzania,

Jengo la Taaluma Na. 1,
Barabara ya Mkalama
S.L.P. 1718
DODOMA,
TANZANIA

Barua pepe: lrct@lrct.or.tz
Tovuti: www.lrct.go.tz

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

# HAKI ZA WATU WENYE ULEMAVU



## 1.0 UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Tume) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171.Kwa mujibu wa sheria hii pamoja na mambo mengine Tume inajukumu la kufanya mapitio ya sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa na kiuchumi na kitekinolojia.

Katika kutekeleza jukumu hili, Tume imefanya mapitio na kuandaa Taarifa ya Mfumo wa Sheria Unaohusu Watu Wenye Ulemavu, 2009.

## 2.0 SHERIA YA WATU WENYE ULEMAVU

Kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume mwaka 2010, Serikali ilitunga Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, Sura ya 287. Sheria hii pamoja na mambo mengine imeanisha masuala mbalimbali yanayohusu watu wenye ulemavu kama ifuatavyo:

### 2.1 Mfuko wa Fedha kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu

Sheria imeanzisha Mfuko wa Fedha wa Taifa kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu. Vyanzo vya fedha za Mfuko ni fedha zinazotengwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Mfuko huu, ada au fedha ambazo zitalipwa katika Mfuko wakati wa kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Watu wenye Ulemavu, fedha yoyote inayotengwa kwa mujibu wa sheria na chanzo chochote kinachotambulika kisheria.

### 2.2 Mfumo wa Usajili wa Watu Wenye Ulemavu

Sheria imempa mamlaka Kamishna wa Ustawi wa Jamii kuanzisha na kutunza rejesta ya watu wenye ulemavu na makazi yao.

### 2.3 Ajira za Watu wenye Ulemavu

Sheria imempa jukumu kila mwaajiri wa sekta ya umma na binafsi kuajiri watu wenye ulemavu ambao wanavigezo kwa ajili ya ajira husika na endapo kuna nafasi ambazo zinafaa watu wenye ulemavu.

### 2.4 Huduma za Afya

Sheria imetoa haki kwa watu wenye ulemavu kupata huduma za afya za kiwango kinachokubalika bila ubaguzi.

### 2.5 Kufikika kwa Majengo

Sheria imempa jukumu Waziri mwenye dhamana ya majengo, kuhakikisha kuwa majengo ya umma na majengo mengine yanayotoa huduma kwa umma yanafikika kwa urahisi kwa watu wote wenye ulemavu. Aidha, Waziri kwa kushauriana na Baraza la Taifa la Ushauri ataandaa Kanuni kuhusu ufikiwaji wa majengo kwa nia ya kutoa muongozo wa taasisi binafsi na za umma.

Sheria inataka kila taasisi ya umma au binafsi kuzingatia utekelezaji wa kanuni hizo hususan wakati wa ujenzi, marekebisho au upanuzi wa majengo ya umma, kila jengo la umma litarekebishwa kwa mujibu wa kanuni za kufikika wa majengo.

### 2.6 Upatikanaji wa Habari

Sheria inazitaka taasisi za umma zinapowasiliana na mtu yoyote au mkuu wa taasisi husika ahakikishe kuwa endapo mawasiliano yanafanyika kwa njia ya mdomo pale ambapo, kuna mtu mwenye ulemavu wa kusikia au kama mawasiliano yanafanyika kwa njia ya maandishi na kuna mtu au watu wenye ulemavu wa kuona, maudhui ya mawasiliano hayo yafikishwe kwa namna ambayo watu wenye ulemavu wataweza kuelewa kadri itakavyowezekana.

Kama taasisi ya umma inawasiliana kwa njia ya kieletroniki na mtu mmoja au zaidi ya mmoja mwenye changamoto ya kuona , mkuu wa taasisi atalazimika kuhakikisha maudhui ya mawasiliano hayo yanafikika kwa kuzingatia teknolojia iliyotengenezwa kwa minajili hiyo.

## 3.0 HITIMISHO

Watu wenye ulemavu wana haki sawa hivyo ni jukumu letu sote kuhakikisha kuwa haki zilizoainishwa katika sheria hii zinatekelezwa kama ilivyokusudiwa.